

**Mambo mengi yanaweza kuingilia afya yako –** kupata muda wa miadi ya daktari; kutafuta na kutayarisha chakula cha bei nafuu, chenye virutubisho vinavyohitajika; kuchukua muda wa kufanya shughuli za ustawi kama vile mazoezi, kutafakari na kujumuika na marafiki; kukumbuka wakati au saa unazopaswa kumeza dawa zako - na mambo mengine mengi.

**Ni sawa ukihisi kwamba unahangaishwa na mambo haya.** Tuko hapa kukusaidia kuelewa kile ambacho huenda kinakuzuia kufanya mambo na kukusaidia kutafuta masuluhisho ili uweze kuzingatia kuboresha afya yako na kuwa na afya njema iwezekanavyo.

## UVM Health
Huduma za Usimamizi wa Utunzaji

**Saa:**
Jumatatu – Ijumaa
Saa 8:00 asubuhi – 4:30 jioni

**Simu**
Bila malipo: 833-763-0652

**Faksi**
802-847-6545

**MyChart**
Ili kupata taarifa ya afya, au kufikia rekodi yako ya matibabu kwa urahisi na usalama kupitia MyChart Mtandaoni, tafadhali tembelea **UVMHealth.org/MyChart** au utupigie simu namba ni **844-886-4325**.

ACCREDITED
NCQA
CASE MANAGEMENT
3 YEARS

**UVMHealth.org**

**Healthier Communities.**
**Healthiest Lives.**
**Together.**

# Huduma za Usimamizi wa Utunzaji

Care Management
SWAHILI



Kusimamia afya yako na kuelewa unapopaswa kwenda ili kupata usaidizi ni kazi ngumu. Hapo ndipo timu yetu ya Huduma za Usimamizi wa Utunzaji inaweza kusaidia.

University of Vermont Health

"Kuwa na mtu mwingine wa kunisikiliza, kunitia moyo, kuwa mshauri na mtu ambaye angeweza kuelewa mambo niliyokuwa nikipitia kulinisaidia sana. Ningependekeza sana mpango huu…"

**— Dondoo kutoka kwa mshiriki wa Huduma za Usimamizi wa Utunzaji**

## Je, ninapataje usaidizi kutoka kwa Huduma za Usimamizi wa Utunzaji?

**Ni muhimu kumjulisha mtoa huduma wako wa afya kuhusu masuala yanayoathiri afya na ustawi wako** au ikiwa unashindwa kufuata mpango wako wa utunzaji. Unaweza kumuuliza mtoa huduma wako ikiwa unaweza kufaidika na usaidizi wa Huduma za Usimamizi wa Utunzaji, au mtoa huduma wako anaweza kukuelezea.

**Msimamizi wa utunzaji atawasiliana nawe ili kupanga mkutano katika mazingira yanayokufaa zaidi –** kwa simu, kwa njia ya video au ana kwa ana. Katika mkutano wa kwanza, msimamizi wako wa utunzaji atauliza kuhusu wasiwasi wako, mambo yanayozuia utunzaji wako na msaada unaohitaji ili kuboresha au kudumisha afya yako.

**Mahitaji yako yanaweza kujumuisha nyanja nyingi,** na msimamizi wako wa utunzaji anaweza kukuunganisha na huduma na mipango ya usaidizi iliyo katika Mfumo wa Afya wa UVM na huduma zilizo katika jamii yako ambazo hatutoi.

**Tutashirikiana nawe kuweka malengo** na kupanga mipango ya kuyafikia. Malengo ya afya yako ni sehemu muhimu ya mpango wako.

## Vipaumbele vyetu ni kukusaidia katika:

- Kuboresha afya yako na ubora wa maisha
- Kushughulikia wasiwasi wako wa muda mrefu wa afya na hali
- Kushirikiana kwa ukaribu na mtoa huduma wako wa msingi na wataalamu
- Kutafuta nyenzo za jamii ili kukusaidia wewe na familia yako

## Je, timu ya huduma za usimamizi wa Utunzaji hufanya nini?

**Timu ya Huduma za Usimamizi wa Utunzaji hufanya kazi kwa karibu na wewe na watoa huduma wako wa afya.**

Pamoja:

- Tutaweka malengo ya kuboresha afya yako
- Tutahakikisha kwamba unaelewa kikamilifu na unaweza kufuata mpango wa utunzaji uliotengenezwa na wewe na mtoa huduma wako
- Tutakagua dawa zako ili tuhakikishe kuwa unajua jinsi ya kuzitumia na kupata machaguo au mipango nafuu zaidi ya kukusaidia kuzilipia.
- Tutakusaidia kupata nafuu na tuhakikishe kuwa una kila kitu unachohitaji baada ya kulazwa hospitalini au katika chumba cha dharura
- Tutatoa machaguo ya huduma za usafiri ili uweze kuhudhuria miadi yako ya matibabu, hasa baada ya kulazwa hospitali au katika chumba cha dharura
- Tutakupa zana, nyenzo na msaada ili kukusaidia kusimamia afya yako

## Je, nani anashiriki katika timu ya Huduma za Usimamizi wa Utunzaji?

**Timu yako ya Huduma za Usimamizi wa Utunzaji inajumuisha:**

- Wewe
- Jina la Mtoa(Watoa) Huduma za Afya
- Familia/mlezi wako (ikiwa yupo)
- Wasimamizi wa utunzaji
- Wataalamu wengine na watoa huduma

## Je, nani anaweza kupokea usaidizi kutoka kwa timu ya Huduma za Usimamizi wa Utunzaji?

**Tunawahudumia watu wazima, watoto, familia, wajawazito, wazee…watu wote!**

## Je, ninapataje manufaa zaidi kutoka kwenye huduma za Usimamizi wa Utunzaji?

**Usaidizi unaopokea kutoka kwa timu ya Huduma za Usimamizi wa Utunzaji utakuwa bora zaidi:**

- Ukitusaidia kukujua Tunaelewa kuwa huenda ikawa vigumu kuzungumza kuhusu afya ya kibinafsi au masuala ya kibinafsi. Kuzungumza na msimamizi wako wa utunzaji kuhusu unachohitaji au kitu chochote kinachozuia utunzaji wako kutatusaidia kukuunganisha na usaidizi unaofaa. Tuko hapa kutoa huduma bora zaidi, bila hukumu.
- Tujulishe ikiwa huelewi kitu au ikiwa una maswali yoyote kuhusu utunzaji wako.
- Tujulishe ikiwa unashindwa kufuata mpango wa utunzaji ambao umetengeneza pamoja na mto huduma wako wa afya.
- Kumjulisha mtoa huduma wako au msimamizi wa utunzaji ikiwa huhitaji huduma hii tena.
- Kama kawaida, tutakutendea kwa heshima na kukuomba ututendee vivyo hivyo.

**Haki na majukumu yako ya mgonjwa yanaweza kupatikana mtandaoni kwenye UVMHealth.org/Care-Management, au unaweza kumwomba msimamizi wako wa utunzaji nakala.**